# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUKAMA 2024

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya Sekondari Bukama,
S.L.P 1
**SHIRATI-RORYA**

Tarehe: 25/04/2024

Mkuu wa Shule: **0784784518**
Makamu Mkuu wa Shule: **0715180854/0786180854**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ______________________________
S.L.P _________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUKAMA KIDATO CHA TANO HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA MKOA WA MARA MWAKA 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 Tahasusi ya ________Shule ya Sekondari Bukama ipo wilaya ya Rorya mkoa wa Mara. Kwa wanaotokea Mwanza wapande mabasi yanayokuja Tarime na washuke **Tarime stendi**,mabasi hayo kwa Mwanza yanapatikana stendi ya **Nyamongoro Mwanza**. Kutoka Tarime stendi wapande magari yanayoelekea **Shirati kupitia Bukama** na washuke **kibao cha shule ya sekondari Bukama**. Kutoka kibao cha shule hadi shuleni ni mita 200 unaweza kutembea kwa miguu.

   Muhula wa masomo unaanza Julai 2024. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe iliyoelekezwa na **OR-TAMISEMI,** mwisho wa kuripoti ni baada ya wiki mbili kama ilivyoelekezwa.

   **NB: UNAPOKUJA HAKIKISHA UNAKUJA NA FOMU HII IKIWA NA MAHITAJI YOTE NA IKIWA IMEJAZWA SEHEMU ZOTE.**

2. **Mambo muhimu ya Kuzingatia**

   2.1 **Sare ya Shule**

   a) Sare ya Shule hii ni mashati mawili (02) meupe ya tetroni yenye mikono mirefu.

   b) Suruali mbili (02) moja rangi ya Khaki No. 1 na nyingine rangi ya ughoro No.1 zenye marinda mawili pande zote. Sare kwa ajili ya kushindia (shamba dress) ambazo ni suruali mbili nyeusi zenye marinda mawili moja kulia na moja kushoto.

   c) Sare ya Michezo bukta rangi ya Bluu ikiwa na T-shirt yake yenye michirizi myeupe (vinapatikana pia duka la shule). Na raba nyeusi jozi moja (01) kwa ajili ya michezo.

   d) Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba nyenye visigino vifupi jozi mbili (02).

   e) Soksi jozi mbili (02) rangi nyeusi zinazovuka kisigino.

   f) Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi jozi mbili (02) na Track suit rangi nyeusi.

g) Masweta mawili(2) moja rangi ya khaki na nyingine rangi ya ughoro (zinapatikana pia kwenye duka la shule zikiwa na nembo ya shule)

h) Nguo za kushindia ni T-shirt mbili (2) moja rangi ya bluu na nyingine kijivu zenye kola yenye michirizi mweupe (zinapatikana pia kwenye duka la shule zikiwa na nembo)

i) Tai jozi mbili(2) moja rangi ya khaki na nyingine rangi ya ughoro zenye nembo ya shule zinapatikana pia duka la shule.

**UVAAJI WA SARE YA SHULE:**

Sare ya shule inavaliwa wakati wote wa masomo. Baraza, Mihadhara, na wakati mwanafunzi anapokwenda nje ya mipaka ya shule . T- shirti ya shule ivaliwe ndani tu wakati usio wa masomo na sweta ivaliwe wakati wa baridi tu. Majaketi, makoti, kofia na mapambo mengine haviruhusiwi kuvaliwa kabisa pamoja na sare ya shule. Hivyo atakaye onekana na mavazi mengine tofauti na yasiyo ainishwa hapo juu atachukuliwa hatua za kinidhamu. Hakuna nguo zitakazo ruhusiwa tofauti na sare za shule.

**2.2 Michango inayotakiwa kulipwa na kila mwanafunzi ni;**

i) Mchango wa uendeshaji wa shule Tsh 65,000/=
ii) Tahadhari Tsh 5000/=
iii) Nembo Tsh 5000/=
iv) Kitambulisho cha shule Tsh 5000/=

Fedha ya michango ya uendeshaji wa shule ilipwe kwenye Akaunti Na. **30401000024**. Benki ya **NMB** Jina la Akaunti **BUKAMA SECONDARY SCHOOL**.
Fedha ya michango ya tahadhari, nembo na kitambulisho ilipwe kwenye akaunti Na. **32810021298 NMB** Jina la Akaunti **BUKAMA SECONDARY SCHOOL ELIMU YA KUJITEGEMEA**

**a) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni;**

i) Ream ya karatasi A4 Double A mbili (2) kwa mwaka
ii) Vitabu vya masomo vya Tahasusi husika.
iii) Scientific calculator silent non programmable with functions Fx – 991MS) kwa wale wanaosoma Tahasusi za EGM na HGE na Mathematical Set.
iv) Godoro kwa wanafunzi wa bweni futi 6 kwa futi 2 $^1/_2$.
v) Mashuka pair 2, (rangi ya bluu) blanket 1, foronya, chandarua 1 (shuka la kimasai hairuhusiwi na halitambuliki kama shuka au blanket).
vi) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
vii) Ndoo mbili kubwa zenye mifuniko.
viii) Kwanja 1, jembe1 lenye mpini, Squeezer 1, soft broom 1, hard broom 1,reki 1 yenye mpini,ufagio1 wa nje wa chelewa wenye mpini, moper 1 na dawa ya chooni ya maji lita 5 aje nayo.
ix) Jalada (file cover) mbili (2) la kutunzia kumbukumbu zako(zinapatikana duka la shule)
x) Vifaa vya usafi (mswaki, dawa ya meno, dawa ya viatu, brashi, kioo, kitana Kandambili, Taulo n.k)

xi) Madaftari (counter Books) yasiyopungua saba (07) madaftari ya kawaida kwa ajili ya mazoezi na graph pad 02
xii) Sanduku imara na kufuri madhubuti kwa ajili ya kutunzia mali zako(tranker)
xiv) Dumu la lita 5 la kutunzia maji ya kunywa kwa kila mmoja.(Anaweza lipata duka la shule.)

3.1 **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa/utoro
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv) kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake/walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) kupigana mwanafunzi kwa mwafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yoyote yule.
vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii) Kufunga ndevu au kufuga nywele
viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix) Uvutaji wa sigara
x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja au kuoa
xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiii) kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xv) Kudharau Bendera ya Taifa
xvi) Kufanya jaribio lolote ya kujiua, au kutishia kama kunywa sumu n.k
xvii) Uharibifu wa Mali ya Umma kwa makusudi.


4. **Viambatanisho na Fomu Muhimu**

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4)za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu **ni za lazima.**
e) Sheria na kanuni za shule ya Sekondari Bukama.
f) Kivuli cha matokeo ya mtihani wa Taifa kidato cha Nne, 2023 (Result Slip)
g) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

5. Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**NB**: **Bima ya Afya:** Hakikisha kijana wako anakuja na Bima ya Afya shuleni kwa ajili ya Matibabu. Kama hana Bima ya Afya atalazimika kulipa Tsh. 50,400/= kwenye akaunti Na. **32810021298 Jina la akaunti BUKAMA SEC SCHOOL ELIMU YA KUJITEGEMEA ambayo** italipwa kwenye mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

***KARIBU SANA KATIKA SHULE HII***



**RICHARD B OKORE**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BUKAMA
S. L. P. 1. SHIRATI
TARIME.

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**MEDICAL EXAMINATION FORM I**

To Medical Officer ..................................................................

....................................................................... Name in Full)

Please examine the above named as to his physical and mental fitness for a Secondary Education.

1. Blood count ..........................................................................................
2. Stool examination ..........................................................................
3. Urine analysis ....................................................................................
4. Venereal disease ..............................................................................
5. T.B and leprosy test .......................................................................
6. Eye sight ..............................................................................................
7. Heating .................................................................................................
8. Asthma ..................................................................................................
9. Epilepsy ...............................................................................................
10. Neuroses .............................................................................................
11. Speech ..................................................................................................
12. Limbs ....................................................................................................
13. Others serious Disease ..............................................................

Remarks and additional information e.g. physical defects or impairments, infection, chronic or family disease e.g. sickle cell.

.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................

I certify that the above named student is fit/is un fit to persue Secondary Education.

Signature ..............................................
Designation..........................................
Station ....................................................
Date and Stamp....................................

**KIAMBATANISHO NA 2**
**TAARIFA BINAFSI**

Unatakiwa kujaza sehemu iliyo wazi, aidha na kusoma kwa makini maelezo yaliyoandikwa.

1. Jina la Mwanafunzi ______________________________________________
2. Anwani yako kamili ______________________________________________
3. Tarehe ya kuzaliwa mwezi na mwaka ____________________________
4. Mahali ulipozaliwa ______________________________________________
5. Dini/Dhehebu ______________________________________________
6. Uraia wako ______________________________________________
7. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ______________ ________________________
8. Anuani ya Mzazi/Mlezi __________________ ______________________
9. Namba ya simu ya Mzazi ________________________________________
10. Mahali anapoishi
    Kijiji __________________________________ Mtaa ________________________

    Kata ________________________________ Wilaya _______________ Mkoa __________

**AHADI**

Mimi ____________________________________________ kwa utashi na akili yangu timamu

ninaikubali nafasi ya masomo niliyopewa, nitakuwa tayari kujiendeleza kimasomo, nimezisoma nimezielewa na nitazifuata sheria za shule pamoja na kanuni na taratibu zitakazotolewa. Natambua kuwa nikifukuzwa shule kwa sababu ya kuvunja sheria za shule kwa makusudi nitavunja moyo wa wazazi na wale wote wanaonisaidia, hivyo jamii itanidharau kabisa. Naahidi kuwa na utii kwa Walimu na Wafanyakazi wote waliopo hapa shuleni ili wanipende na kunisaidia zaidi. Sitakuwa tayari kuanzisha kushauri wala kushiriki katika vurugu za aina yoyote hapa shuleni hususani mgomo kwani ni kwenda kinyume na sheria na taratibu za shule. Nitakuwa na utii na viongozi wa shule na upendo wa wanafunzi wenzangu wote. Pia nitafanya bidii katika masomo na kazi zote za shule.

***MUNGU NISAIDIE***

| ______________________________ | ________________________ | _________________ |
|---|---|---|
| **JINA NA SAINI YA MZAZI/MLEZI** | **SAINI YA MWANAFUNZI** | **TAREHE** |

**KIAMBATANISHO NA. 3**

**MAELEOZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI**

Sehemu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi:

1. Jina la Mzazi/Mlezi 1:…………………………………………………………… Na. ya simu………………………

2:……………………………………………………………Na. ya simu………………………..

2. Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni

1:……………………………………………………………………………………….. Na. ya simu……………………

2:……………………………………………………………………………………….. Na. ya simu……………………

| Mzazi: 1 | Mzazi: 2 | Ndugu: 1 | Ndugu: 2 |
|---|---|---|---|

3. Anwani ya mahali na Mtaa unapoishi sasa …………………………………………………………
4. Mahalipo ulipozaliwa Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………..
5. Kazi ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………………..
6. Dini au Dhehebu la Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………
7. Uraia Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………………..

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

- Nitashirikiana na Uongozi wa Shule katika suala la kumlea, kumwendeleza au kumtia moyo wa kupenda Shule.
- Nitamsaidia mtoto wangu vifaa vya shule ambavyo havitolewi shuleni
- Nitahakikisha kwamba mtoto wangu anawahi shuleni na pia hachelewi likizoni.
- Nitafuatilia maendeleo yake kwa karibu zaidi ikibidi hata kuonana na walimu wake.
- Ninatambua pia kumchelewesha kufika shuleni siku ya kufungua shule kunaweza kusababisha kupoteza nafasi aliyopewa.
- Nitamruhusu/nitamleta mwanafunzi kuripoti akiwa amekamilisha mahitaji yote.

8. Jina la Balozi .......................................................................................... Saini/Mhuri......................................
Tarehe ......................................... Namba ya Simu ...................................................

9. Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji ............................................................ Saini ……………………..
Tarehe................................ Namba ya Simu ...................................... Mhuri.............................................

Saini ya Mzazi/Mlezi 1:........................................................................ Tarehe.............................
Saini ya Mzazi/Mlezi 2: ....................................................................... Tarehe ............................

*NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA*

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BUKAMA
S.L.P. 1. SHIRATI
TARIME.

**MKUU WA SHULE:**

**KIAMBATANISHO NA. 4**

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI BUKAMA**

Sheria hizi zinalenga **UTII, HESHIMA NA NIDHAMU**.

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimu Mwalimu, mtu yeyote au kundi la watu wanaomzidi umri popote awaonapo au kukutana nao.
2. Ni marufuku kutumia lugha chafu wakati wowote kwa walimu, wao kwa wao na watu wengine.
3. Unatakiwa kuheshimu alama za Taifa mfano **Bendera ya Taifa, Viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa.**
4. Hauruhusiwi kuonekana au kutembelea:
   a) Vilabu vya Pombe
   b) Kumbi za Starehe (kama zipo)
   c) Nyumba za kulala wageni
   d) Nyumba za walimu/watumishi bila ruhusa.
5. Hauruhusiwi kuharibu Mali ya Shule, ni **kosa zito**.
6. Kuzingatia usafi binafsi na kuhifadhi mazingira ya shule
7. Hauruhusiwi kupiga kelele ovyo ndani na nje ya Madarasa
8. Unatakiwa kutumia Kiingereza daima wakati wote ndani na nje ya darasa.
9. Ni marufuku kabisa kwa mwanafunzi:
   (a) Kuvuta sigara au kunywa Pombe
   (b) Kufuga kucha au kuzipaka rangi
   (c) Kufuga ndevu na nywele ndefu
   (d)Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
   (e) Kugombana ama kupigana
   (f) Kutoroka darasani au kazini
   (g) Kuvaa kofia au Bangili na Mapambo mengine yasiyo ya lazima
   (h) Kuiga mitindo ya kihuni mfano mavazi, kunyoa kipara, kusuka nywele kwa wasichana
   (i) Kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa.
10. Unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani na kufanya mazoezi, Majaribio na Mitihani yote inayotolewa na Mwalimu.
11. Wakati wa vipindi hauruhusiwi kwenda nje ya shule bila ruhusa.
12. Ni lazima kuvaa sare ya shule kila uwapo katika eneo la shule.
13. Mwanafunzi atakaye kutwa au kubainika kutoroka na kwenda nje ya shule bila ruhusa atakuwa ameshiriki kukata na kuharibu uzio wa shule hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kulipa gharama za uharibifu huo au kufukuzwa shule.
16. **Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi. Endapo mwanafunzi atakutwa au kukamatwa na simu shuleni hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule mara moja.**
17. Mwanafunzi anatakiwa kuitikia wito wa kengele kwa kukimbia na kuwahi kila anapohitajika.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kulala bwenini wakati wa vipindi vya darasani.

19. Mabweni yanatakiwa kufungwa wakati wote wanafunzi wawapo darasani.
20. Taa za Bwenini zinatakiwa kuzimwa saa 1:00 asubuhi na kuwashwa saa 1:00 usiku tu.
21. Wanafunzi hawaruhusiwi kufanya vikao bwenini bila ruhusa ya mwl. mlezi wa Bweni.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI**:

(a) Uasherati

(b) Wizi

(c) Ubakaji na ushoga

(d) Makosa ya Jinai

(e) Uvutaji Bangi na matumizi ya Madawa ya Kulevya

(f) Kupigana au kupiga

(g) Kudharau Bendera ya Taifa

(h) Kuoa au kuolewa

(i) Kupata Mimba au kusababisha Mimba ndani na nje ya Shule

(j) Kutoa Mimba

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo zenye kuvuruga amani na usalama wa watu

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi

(ℓ) Mwanafunzi kuwa na Simu ya Mkononi Shuleni.

**NB: Unashauriwa muda wote kutumia busara ya kuzaliwa ili uweze kutenda mambo yanayozingatia Sheria na Taratibu zote za Shule.**

..................................

**RICHARD B OKORE**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BUKAMA
S.L.P. 1. SHIRATI
TARIME.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**


- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

# ZINGATIA

**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI /MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0784 784 518**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0715 180 854 AU 0786 180 854**
- **Mwandamizi Taaluma : 0765 564 482**
- **Patron: 0627 778 894**



MKUU WA SHULE

